Eastern Africa Journal of
Contemporary Research (EAJCR)

# *Tathmini ya Mbinu za Mawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili chini ya Elimu ya Mtaala wa Umilisi na Utendaji (CBC) katika Vyuo vya Ualimu, Kenya*

Peter Karanja na Evelyne Kakivi Muthui

## Article information:

To cite this article:

Karanja, P.& Muthui, E. K. (2025). *Tathmini ya Mbinu za Mawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili chini ya Elimu ya Mtaala wa Umilisi na Utendaji (CBC) katika Vyuo vya Ualimu, Kenya. Eastern Africa Journal of Contemporary Research, 5*(2), 198-206.

## For Authors

If you would like to publish your conceptual/theoretical and empirical research articles, case studies and book reviews with EAJCR, please use for authors information about how to write your work and submission guidelines. Please, visit https:// www.eajcr.org/

## About Eastern Africa Journal of Contemporary Research (EAJCR)

The Eastern Africa Journal of Contemporary Research (EAJCR) is both an online (ISSN: 2663-7367) and print (ISSN: 2663-7359) double-blind peer-reviewed quarterly journal published by the Directorate of Research and Publications of Gretsa University, Kenya.

EAJCR aims at advancing the frontiers of knowledge by publishing contemporary multidisciplinary conceptual/ theoretical and empirical research articles as well as case studies and book reviews.

Vol. 5, Issue 2, 2025, ISSN: 2663-7367 (Online) & ISSN: 2663-7359

# Tathmini ya Mbinu za Mawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili chini ya Elimu ya Mtaala wa Umilisi na Utendaji (CBC) katika Vyuo vya Ualimu, Kenya

**Peter Karanja**
Department of Languages, Literature, and Communication Studies
Gretsa University
Thika, Kenya
karanjap@gmail.com

**Evelyne Kakivi Muthui**
Department of Kiswahili
Kitui Teachers Training College
Kitui, Kenya
Klyn2030@gmail.com

## Muhtasari

*Utafiti huu ulitathmini ufanisi wa mbinu za mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili chini ya Mtaala wa Umilisi na Utendaji (CBC), kwa kuangazia mazingira ya Chuo cha Ualimu cha Kitui kama mfano wa taasisi za mafunzo ya ualimu nchini Kenya. Kwa kutumia muundo wa mbinu mseto, data za kiasi zilikusanywa kutoka kwa wanafunzi wa ualimu (N = 120) na walimu wa Kiswahili (N = 12) kupitia dodoso la Likert. Data za ubora zilipatikana kupitia mahojiano ya kina na uchanganuzi wa nyaraka za ufundishaji wa Kiswahili. Matokeo yalionyesha matumizi ya kiwango cha kuridhisha ya mbinu shirikishi kama majadiliano ya kikundi, uigizaji, shughuli za mwingiliano, uandishi wa ubunifu, na mawasiliano ya kimatendo. Uchanganuzi wa takwimu ulionyesha uhusiano wa wastani wa nguvu kati ya kiwango cha matumizi ya mbinu shirikishi na utendaji wa wanafunzi ($r = 0.47$, $p < 0.05$). Changamoto kubwa zilijumuisha upungufu wa vifaa vya kufundishia, msongamano wa madarasa, muda mdogo wa vipindi, na ukosefu wa mafunzo endelevu kwa walimu. Utafiti unahitimisha kuwa mbinu za mawasiliano ni msingi wa kufanikisha CBC, lakini zinahitaji mazingira wezeshi, uwekezaji wa TEHAMA, na mafunzo endelevu ya walimu. Mapendekezo yanasisitiza hitaji la sera madhubuti, rasilimali stahiki, na tathmini ya kiutendaji inayolenga kujenga umahiri wa lugha miongoni mwa wanafunzi wa ualimu.*

***Maneno muhimu:*** *CBC, mbinu za mawasiliano, Chuo cha Ualimu cha Kitui, ufasaha wa lugha, Communicative Language Teaching, uandishi wa ubunifu*

## 1. Utangulizi

Msukumo wa kimataifa wa kujenga jamii yenye maarifa zaidi na kuongeza ushindani katika masoko ya ajira umepelekea kuanzishwa kwa mitaala badalia yenye lengo la kutafuta elimu muafaka zaidi. Kulingana na Amutabi (2019), mwelekeo wa umahiri katika elimu unalenga kushughulikia pengo lililopo kati ya mahitaji ya wafanyakazi wenye ujuzi na upatikanaji wao. Pia, kasi kubwa ya utandawazi na maendeleo ya teknolojia imehitaji mabadiliko katika mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ili kukidhi mahitaji ya stadi muhimu katika karne ya 21 (Barasa, 2021).

Nchini Kenya, kumeanzishwa Mtaala wa Umilisi na Utendaji (*Competency-Based Curriculum* - CBC) ambao umenuiwa kuleta mageuzi muhimu katika ufundishaji, ikiwemo ufundishaji wa lugha nchini Kenya (KICD, 2019). Kwa kurejelea ufundishaji wa lugha, CBC inasisitiza matumizi ya lugha katika mazingira halisi badala ya kujifunza kwa nadharia pekee. Mtaala huu unamtambua mwanafunzi kama mshiriki hai anayejifunza lugha kwa kupitia mazungumzo, utatuzi wa matatizo, mawasiliano ya kimatendo, na ubunifu. Kulingana na KICD, katika ufundishaji wa Kiswahili, CBC inasisitiza umuhimu wa mbinu shirikishi zinazojenga ujuzi, stadi, na mitazamo inayowezesha mwanafunzi kutumia lugha kwa ufasaha katika mazingira ya kijamii, kitaaluma, na kitaifa (KICD, 2019).

Vyuo vya ualimu vina nafasi ya kipekee katika kuhakikisha mafanikio ya CBC kwa sababu vinamtayarisha mwalimu wa kufanikisha malengo ya mfumo huu. Kuna haja ya kuzua na kufanikisha mikakati ambayo itahakikisha walimu wametayarishwa vyema katika vyuo vya ualimu ili nao waweze kufanikisha malengo ya CBC katika shule watakazokuwa wanafunza.

Utafiti huu ulichunguza mbinu zinazotumiwa katika kutayarisha walimu wa Kiswahili katika kukidhi matarajio ya mfumo wa CBC. Utafiti pia umechunguza changamoto zinazojitokeza katika harakati hizi za kuwatayarisha walimu wa Kiswahili. Kwa kuwa CBC inazingatia ufunzaji na ujifunzaji katika mazingira halisi badala ya kujifunza kwa nadharia pekee, utafiti huu umezingatia Mbinu ya Mawasiliano ya Ufunzaji wa Lugha (*Communicative Language Teaching* - CLT) ya lugha ambayo inasisitiza ujifunzaji wa lugha katika mazingira halisi. Utafiti umejikita katika mazingira halisi ya Chuo cha Ualimu cha Kitui. Machulio ni kuwa, mwanafunzi wa ualimu wa Kiswahili katika Chuo cha Ualimu cha Kitui anapaswa kutayarishwa kwa kuzingatia mbinu shirikishi, mintarafu zile zinazozingatiwa na nadharia ya CLT. Utafiti umeangazia pia changamoto zinazokabili harakati za kumtayarisha mwanafunzi wa ualimu katika Chuo cha Ualimu cha Kitui.

## 2. Mapitio ya Maandishi

### 2.1 Mtaala wa CBC na Ufundishaji wa Lugha

Mtaala wa Umilisi (Competency-Based Curriculum – CBC) ni mfumo wa elimu unaolenga kukuza ujuzi, stadi, maadili na mielekeo inayomwezesha mwanafunzi kufanya kazi za maisha ya kila siku kwa ufanisi. Kulingana na Taasisi ya Kuendeleza Mitaala ya Kenya (KICD), CBC inalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri unaomsaidia kutatua changamoto za mazingira yake kwa kutumia maarifa na ujuzi aliopata shuleni (KICD, 2017). Hivyo, CBC inajikita katika kuimarisha uwezo bali siyo kukariri maarifa pekee.

Mtaala wa CBC unasisitiza kujifunza kwa vitendo, ubunifu, na uhusiano wa maudhui ya somo na mazingira halisi ya mwanafunzi (KICD, 2019). Kwa kurejelea Kiswahili, mwanafunzi anatarajiwa kuwa mfasaha, mwenye uwezo wa kuandika na kuzungumza kwa kujiamini, na kutumia sarufi katika matumizi ya kimuktadha ya lugha (KICD, 2019). Ufundishaji wa lugha kwa mtazamo huu unahitaji mbinu shirikishi inayomweka mwanafunzi katikati ya ujifunzaji kama vile Mbinu ya Mawasiliano ya Ufunzaji wa Lugha (CLT).

.

## 2.2 Mbinu ya Mawasiliano ya Ufunzaji wa Lugha (CLT)

Mbinu ya Mawasiliano ya Ufunzaji wa Lugha (Communicative Language Teaching – CLT) ina misingi yake katika nadharia ya Umahiri wa Mawasiliano iliyoasisiwa na Hymes mwaka wa 1972. Huu ni mkabala wa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha unaosisitiza kuwa lengo kuu la kujifunza lugha ni kupata "umahiri wa mawasiliano" badala ya umahiri wa kisarufi pekee (Hymes, 1972). Kwa mtazamo huu, kujua lugha si tu kujua kanuni zake (sarufi), bali pia ni kujua nini cha kusema, kwa nani, na katika mazingira gani. Kwa kurejelea Kiswahili, Richards (2006) anafafanua kuwa maana ya CLT ni kumwezesha mwanafunzi kutumia Kiswahili kama chombo cha kutatua matatizo na kujenga mahusiano, badala ya kukichukulia kama somo la kukaririwa darasani.

Mbinu ya kufundisha lugha ya CLT huzingatia mawasiliano kama lengo kuu la kujifunza lugha (Richards na Rodgers, 2014). Mbinu hii ya CLT ni mkabala wa ufundishaji lugha unaosisitiza kuwa lengo kuu la kujifunza lugha ni umahiri wa mawasiliano (*communicative competence*). Badala ya mwanafunzi kukariri kanuni za lugha, kama vile sarufi na msamiati, pekee, anafundishwa jinsi ya kutumia lugha hiyo kupitisha ujumbe, kueleza hisia, na kushirikiana na wengine katika mazingira halisi. Kulingana na Richards na Rodgers (2001), mbinu ya CLT inasisitiza kuwa lugha ni mfumo wa kuelezea maana na kuwa ufundishaji wa Kiswahili unapaswa kulenga uwezo wa mwanafunzi kuwasilisha ujumbe badala ya kukariri sheria pekee.

Nunan (1991) anakariri kuwa mwanafunzi ndiye mshiriki mkuu katika mchakato wa kujifunza. Hii ina maana kuwa walimu wa lugha kama Kiswahili wanapaswa kupunguza muda wao wa kuzungumza na kufunza nadharia na badala yake kuwapa wanafunzi nafasi zaidi ya kutumia lugha darasani. Katika CLT, mwalimu ni mwezeshaji, mshauri, na msimamizi wa shughuli za darasani (Richards na Rodgers, 2014) na kazi yake kuu ni kuandaa mazingira ambayo yanamlazimu mwanafunzi kutumia lugha kuwasiliana[55]. Kwa upande wa pili, mwanafunzi ni mshiriki hai. Anapaswa kushiriki kupitia harakati kama vile majadiliano, uigizaji, na kazi za kikundi. Ong'onda na Musi (2022) wanasisitiza kuwa katika darasa la Kiswahili, mwanafunzi anawajibika "kujaribu" kutumia lugha hata kama atafanya makosa, kwani makosa yanachukuliwa kama sehemu ya kujifunza.

Mbinu ya CLT pia inahimiza utumizi wa vifaa visaidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha. Mbinu hii haiegemei kwenye vitabu vya kiada pekee, bali inasisitiza matumizi ya vifaa halisi kama vile magazeti, matangazo ya redio, au maigizo ya maisha ya kila siku (Nunan, 1991). Larsen-Freeman (2000) anasema kuwa matumizi ya vifaa halisi (kama vile magazeti ya Kiswahili, redio, au matangazo) humsaidia mwanafunzi kukabiliana na lugha halisi inayoishi, badala ya lugha ya vitabuni iliyorahisishwa. Kwa mtazamo huu, mafunzo ya walimu katika vyuo vya ualimu yanapaswa kuhimiliwa kwa miundo mbinu na vifaa vya kutosha katika kujifunza jinsi ya kufundisha lugha.

Katika ufundishaji wa Kiswahili, upeo wa CLT unajumuisha stadi zote nne: kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika, lakini kwa msisitizo mkubwa kwenye mwingiliano. Mutiso (2023) anabainisha kuwa upeo wa CLT katika Mtaala wa CBC unalenga "lugha katika muktadha," ambapo mwanafunzi anajifunza sarufi (kama ngeli na minyambuliko) kupitia matumizi yake katika sentensi na mazungumzo, na si kwa kukariri sheria. Tafiti

nyingi (Achieng, 2021; Mutiso, 2023; Richards, 2006; Ringo, 2025; Wambua, 2022) zinaonyesha kuwa CLT huongeza ufasaha wa lugha, kujiamini, na uwezo wa wanafunzi kushiriki katika mawasiliano ya kimuktadha. Hata hivyo, tafiti nyingi kati ya hizi zimejikita zaidi katika mazingira ya shule, kinyume na mazingira ya vyuo vya ualimu yaliyolengwa katika utafiti huu. Waalimu ni watekelezaji wa mfumo wa CBC na kwa hivyo mafunzo yao yanapaswa kuangaziwa katika kiwango cha ufaulifu, mintarafu malengo ya CBC.

Kwa msingi huu, utafiti uliongozwa na haja ya kuelewa kwa kina jinsi mbinu za mawasiliano zinavyotekelezwa katika ufundishaji wa Kiswahili katika Chuo cha Ualimu cha Kitui, namna zinavyoboresha utendaji wa wanafunzi wa ualimu, na jinsi walimu na wanafunzi wa ualimu wanavyotazama ufanisi wake katika mazingira ya CBC. Utafiti pia ulilenga kubainisha vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji kamili wa mbinu shirikishi. Kupitia uchunguzi wa kina wa matumizi ya mbinu shirikishi, athari zake kwa ufasaha wa wanafunzi, mitazamo ya walimu kuhusu faida na changamoto zake, pamoja na uchambuzi wa vikwazo vinavyotokana na mazingira ya ufundishaji, utafiti huu unatoa ushahidi adilifu unaoweza kuimarisha mafunzo ya walimu wa lugha ya Kiswahili na kuboresha utekelezaji wa CBC nchini Kenya.

### 2.3 Changamoto za utekelezaji wa CLT

Ingawa mbinu za mawasiliano, kamavile Mbinu ya Mawasiliano ya Ufunzaji wa Lugha (CLT), zimependekezwa sana na wataalamu katika mfumo wa CBC nchini Kenya, tafiti nyingi zinadhihirisha mwanya mkubwa kati ya nadharia na utekelezaji wake. Kuna changamoto katika utekelezaji wake kama vile upungufu wa vifaa, ukosefu wa mafunzo endelevu kwa walimu shuleni, msongamano wa madarasa, na ukosefu wa ufadhili wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), miongoni mwa nyingine (Chebet, 2020; Kilonzo, 2022; Mwangi na Otieno, 2022; Onchwaria, 2020). Hali hii imedhoofisha jitihada za utekelezaji wa CBC. Baadhi ya tafiti hizi zililenga shule za upili. Hata hivyo, utafiti huu ulizingatia kuchunguza hali ilivyo katika kufunza na kujifunza Kiswahili chini ya mtaala wa CBC kwa kutumia mbinu ya CLT katika Chuo cha Ualimu cha Kitui.

## 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Chuo cha Ualimu cha Kitui katika Kaunti ya Kitui nchini Kenya. Hiki ni mojawapo kati ya vyuo vingi vya ualimu nchini Kenya vinavyotayarisha walimu wa shule za msingi. Vyuo vyote vya ualimu hutumia mtaala sawa wa masomo na kwa hivyo matokeo ya utafiti katika chuo kimoja yanaweza kuangazia hali ilivyo katika vyuo vingine kwa kiwango kikubwa.

Utafiti huu ulitumia muundo wa mbinu mseto (Creswell na Creswell, 2018). Utafiti uliunganisha takwimu za kiasi na data za ubora ili kupata taswira pana na ya kina kuhusu ufanisi wa mbinu za mawasiliano katika ufundishaji wa Kiswahili Chuo cha Ualimu cha Kitui. Washiriki walijumuisha walimu kumi na wawili wa Kiswahili (N=12) pamoja na wanafunzi wa ualimu mia moja na ishirini (N=120). Mchanganyiko wa makundi haya uliwezesha kukusanya taarifa zinazotafakari uzoefu wa moja kwa moja wa walimu na mitazamo ya wanafunzi kuhusu mbinu za ufundishaji chini ya CBC.

Katika utekelezaji wake, utafiti ulifuata Muundo wa Mbinu Mseto wa Kifafanuzi wa Kimfuatano (*explanatory sequential mixed-methods*). Ukusanyaji wa data za kiasi ulitangulia, ukifuatiwa na uchambuzi wa kina wa data za ubora ili kufafanua kwa undani matokeo ya awali. Mbinu hii iliruhusu kulinganisha takwimu na maelezo ya kina, hivyo kuimarisha uhalali wa hitimisho la utafiti. Walimu waliteuliwa kimakusudi kwa kutumia Usampulishaji wa Kimakusudi, ilhali wanafunzi walichaguliwa kwa mbinu ya nasibu rahisi.

Ukusanyaji wa data ulitegemea vyombo vitatu vya utafiti:

- Dodoso la Likert (1–5): Kwa wanafunzi ili kupima kiwango cha matumizi ya mbinu shirikishi, athari zake kwa ujifunzaji, na changamoto zinazojitokeza.
- Mahojiano ya kina**:** Kwa walimu wa Kiswahili ili kuchunguza uzoefu wao wa ufundishaji, utayari wao katika kutekeleza CBC, na mtazamo wao kuhusu ufanisi wa mbinu shirikishi.
- Uchanganuzi wa nyaraka: Ulihusisha mihtasari ya masomo, Vitini vya ufundishaji, na mwongozo wa CBC wa KICD ili kuchunguza kama mbinu za mawasiliano zimejengwa ipasavyo katika maandishi ya ufundishaji.

Uhalali wa vyombo vya utafiti ulithibitishwa kupitia tathmini ya wataalamu wa elimu ya lugha kutoka Chuo cha Ualimu cha Kitui. Uaminifu wa dodoso ulipimwa kwa kutumia *Cronbach's Alpha* ambapo thamani ya 0.82 ilipatikana. Data za kiasi zilichambuliwa kwa kutumia *SPSS* kupitia asilimia, wastani na uhusiano wa *Pearson (r)*. Data za ubora zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya *thematic analysis*.

## 4. Matokeo na Majadiliano

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua matokeo ya utafiti kulingana na malengo yake makuu.

### 4.1 Matumizi ya Mbinu za Mawasiliano katika Ufundishaji

Matokeo yanaonyesha kuwa walimu wa Kiswahili Chuo cha Ualimu cha Kitui wanatumia mbinu za mawasiliano kwa kiwango cha kuridhisha, japo matumizi hutofautiana kulingana na aina ya shughuli na rasilimali zilizopo. *Jedwali 1* linaonyesha uwiano wa mbinu zinazotumiwa na walimu na maelezo mafupi ya matumizi yake darasani.

**Jedwali 1: Matumizi ya Mbinu za Mawasiliano (N = 12)**

| Mbinu | % ya walimu | Maelezo |
|---|---|---|
| Majadiliano ya kikundi | 83% | Hutawala katika masomo ya mijadala na uchambuzi wa maandishi |
| Uigizaji | 75% | Hutumika katika kufundisha sarufi ya kimuktadha, mazungumzo na matamshi |
| Maswali–Majibu | 67% | Hutumika zaidi kwa mada ngumu kama sintaksia na semantiki |
| Uandishi wa ubunifu | 59% | Hufanya sehemu ya tathmini ya utendaji na ubunifu wa lugha |
| TEHAMA | 41% | Matumizi yake hupunguzwa na upatikanaji hafifu wa vifaa |
| Maelezo (*lecture*) | 24% | Hutumiwa zaidi katika upungufu wa muda au msongamano wa darasa |

Matokeo haya yanaonyesha wazi kuwa mbinu shirikishi ndizo zinazotawala ufundishaji wa Kiswahili katika chuo, jambo linaloendana na matarajio ya CBC ambayo yanahitaji mwanafunzi awe mshiriki hai wa ujifunzaji. Walimu wengi walisema majadiliano ya kikundi na uigizaji yanaongeza kujiamini kwa wanafunzi na hurahisisha kufundisha sarufi kwa kutumia muktadha halisi. Hata hivyo, baadhi yao waliashiria kuwa uandishi wa ubunifu na TEHAMA bado havitumiki kikamilifu kutokana na changamoto za vifaa na muda.

### 4.2 Uhusiano kati ya Matumizi ya Mbinu za Mawasiliano na Ufaulu wa Wanafunzi

Uchanganuzi wa takwimu za wanafunzi ulionyesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya kiwango cha matumizi ya mbinu shirikishi na ufaulu wa wanafunzi katika mawasiliano ya mdomo na uandishi wa kivitendo.

**Jedwali 2: Ufaulu wa Wanafunzi kwa Kazi za Mawasiliano ($N = 120$)**

| Kiwango cha Matumizi | Mazungumzo (%) | Uandishi (%) | *Pearson r* |
|---|---|---|---|
| Juu (Likert 4.3) | 73 | 70 | 0.47* |
| Wastani (Likert 3.1) | 61 | 58 | — |

*$p < 0.05$

Matokeo yanaonyesha uhusiano wa wastani wenye umuhimu wa kitakwimu ($r = 0.47$), jambo linaonyesha kuwa kadri walimu wanavyotumia mbinu shirikishi zaidi, ndivyo ufaulu wa wanafunzi unavyoongezeka. Sababu ya uhusiano huu inaeleweka kupitia nadharia ya *Communicative Competence* ya Hymes (1972) inayodai kuwa umahiri wa lugha haujengwi kwa maarifa ya kanuni pekee, bali kupitia matumizi ya lugha katika mazingira ya kijamii na kiutendaji.

Hali hii inaonekana katika tabia ya wanafunzi waliopata alama za juu: walionyesha kujiamini zaidi katika mazungumzo ya kidadisi, waliweza kutumia miundo ya kisarufi kwa muktadha sahihi, na walionyesha ubunifu zaidi katika kazi za uandishi.

### 4.3 Changamoto Zinazoathiri Utekelezai wa Mbinu za Mawasiliano

Walimu walibainisha changamoto kadhaa zinazokwamiza utekelezaji thabiti wa mbinu shirikishi. Changamoto hizo zimewasilishwa katika *Jedwali 3.*

**Jedwali 3: Changamoto Zinazokumba Ufundishaji kwa kutumia CLT ($N = 12$)**

| Changamoto | % Waliotaja |
|---|---|
| Uhaba wa vifaa vya kufundishia | 82% |
| Msongamano wa madarasa | 76% |
| Muda mdogo wa kufundishia | 68% |
| Ukosefu wa mafunzo endelevu | 63% |
| Mitazamo hasi kuhusu mbinu mpya | 41% |

Uchanganuzi unaonyesha kuwa changamoto hizi zinatokana zaidi na miundombinu duni na ukosefu wa usaidizi wa kitaasisi kuliko ukosefu wa motisha ya walimu. Walimu waliolalamikia msongamano wa madarasa walionyesha kuwa shughuli kama uigizaji na majadiliano ya kikundi zinahitaji nafasi na muda wa kutosha ili kutekelezwa kikamilifu.

**Mchoro 1: Uhusiano kati ya Matumizi ya Mbinu na Ufaulu**

Mchoro wa kutawanyika unaonyesha mwelekeo chanya: kadri kiwango cha matumizi ya mbinu shirikishi kinavyoongezeka, ndivyo ufaulu wa wanafunzi unavyopanda.

```
Ufaulu (%)
80 |              *
75 |             *
70 |          *
65 |        *
60 |      *
55 |    *
50 |   *
45 |  *
----------------------------------------
   2.5   3.0   3.5   4.0   4.5
```

**Kiwango cha Matumizi (Likert)**

Mwelekeo huu unathibitisha matokeo ya *Jedwali 2* na kuunga mkono dhana kwamba ufundishaji unaotegemea mwingiliano wa kimatendo unaongeza uelewa wa sarufi, msamiati, ufasaha na uandishi.

### 4.4 Majadiliano ya Jumla

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa Chuo cha Ualimu cha Kitui kimepiga hatua katika kupokea na kutekeleza mbinu za mawasiliano, na kwamba mbinu hizi zina athari chanya katika kukuza umahiri wa wanafunzi wa ualimu. Matokeo haya yanawiana na madai ya Richards (2006) kuwa CLT huchochea matumizi hai ya lugha na huongeza motisha wa wanafunzi. Aidha, yanathibitisha nadharia ya Hymes (1972) kuhusu kujenga umahiri wa mawasiliano kupitia matumizi. Hata hivyo, mafanikio ya CLT hayawezi kutegemea mbinu pekee; yanahitaji mazingira ya ufundishaji yenye rasilimali za kutosha, mafunzo endelevu ya walimu, na ratiba inayotambua umuhimu wa shughuli za kivitendo. Changamoto kuu ziko katika miundo mbinu na upatikanaji wa vifaa vya kufunzia.

Hata hivyo, changamoto zilizotambuliwa zinaonyesha kuwa mafanikio ya CLT hayawezi kutegemea mbinu pekee; yanahitaji mazingira ya ufundishaji yenye rasilimali za kutosha, mafunzo endelevu ya walimu, na ratiba inayotambua umuhimu wa shughuli za kivitendo. Hivyo, ili kuboresha utekelezaji wa CBC, ni muhimu vyuo kama Chuo cha Ualimu cha Kitui kuwekeza katika miundombinu, TEHAMA, na usaidizi wa kitaaluma unaoendana na mahitaji ya CLT.

## 5. Hitimisho

Utafiti huu umedhibitisha kuwa hatua kubwa zimepigwa katika kushirikisha malengo ya CBC katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika vyuo vya ualimu. Hii imewezeshwa na utumizi wa mbinu ya ufunzaji wa CLT amabyo imeonekana kufaulu kwa kiwango kikubwa katika Chuo cha Ualimu cha Kitui. Hata hivyo, licha ya kuwango hiki cha kuridhisha cha

utumizi wa mbinu muafaka za kufundisha Kiswahili kwa walimu, imebainika kuwa kungali na changamoto zinazohusiana na upungufu wa visaidizi vya ufunzaji na ujifunzaji. Imebainika wazi kuwa mbinu za mawasiliano ni msingi wa kufanikisha CBC katika ufundishaji wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha wazi kuwa matumizi thabiti ya mbinu shirikishi huongeza ufasaha, msamiati, sarufi ya kimuktadha, na ujasiri wa wanafunzi. Hata hivyo, mafanikio haya yanahitaji mazingira wezeshi, uwekezaji wa rasilimali, TEHAMA, na mafunzo endelevu ya walimu. Kwa vile mtaala wa mafuzo katika vyuo vyote vya ualimu ni sawa, mahitimisho haya yanaweza kuhusishwa na vyuo vyote vya ualimu Kenya kwa kiwango kikubwa.

## Marejeleo


Achieng, L. (2021). *Changamoto za utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi katika ufundishaji wa lugha za Kiafrika*. Jomo Kenyatta University Press

Amutabi, M. N. (2019). Competency-Based Curriculum and the challenge of job-market mismatch in Kenya. *International Journal of Education and Social Science Research, 2*(1), 123–140.

Barasa, J. (2021). The impact of globalization and technology on curriculum reform in Kenya: A focus on 21st-century skills. *Journal of Education and Technology, 15*(4), 88–105

Chebet, R. (2020). Teacher preparedness in implementing competency-based curriculum in Kenya. *Journal of Education and Practice, 11*(4), 45–56.

Creswell, J. W., & Creswell, J. D. (2018). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (5th ed.). Sage.

Hymes, D. (1972). On communicative competence. In J. Pride & J. Holmes (Eds.), *Sociolinguistics: Selected readings* (pp. 269–293). Penguin.

Kenya Institute of Curriculum Development. (2017). *Basic Education Curriculum Framework*. Nairobi, Kenya: Author.

Kenya Institute of Curriculum Development (KICD). (2019). *Competency Based Curriculum: Teacher Education Framework*. Nairobi: Government Printer.

Kilonzo, P. (2022). Utekelezaji wa mbinu shirikishi katika kufundisha Kiswahili: Uchunguzi katika vyuo vya ualimu. *Journal of Language Education, 7*(2), 113–128.

Larsen-Freeman, D. (2000). *Techniques and principles in language teaching* (2nd ed.). Oxford University Press.

Mutiso, J. (2023). Mawasiliano na umahiri wa lugha katika vyuo vya ualimu: Uchanganuzi wa CBC. *East African Journal of Educational Studies, 5*(1), 33–50.

Mwangi, P., & Otieno, C. (2022). Implementation of the competency-based curriculum in teacher training colleges in Kenya. *African Journal of Education Research, 9*(3), 201–220.

Nunan, D. (1991). *Language teaching methodology*. Prentice Hall.

Onchwaria, T. N. (2020). *Implementation of the competency-based curriculum in teacher training colleges in Kenya* [Master's Thesis, Kenyatta University]. KU Repository.

Ong'onda, N., & Musi, L. (2022). Changamoto na Matarajio ya Ufundishaji wa Fasihi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari za Kenya. *Jarida la Taaluma za Kiswahili, 10*(1), 112-135.

Richards, J. C. (2006). *Communicative language teaching today*. Cambridge University Press.

Richards, J. C., & Rodgers, T. S. (2001). *Approaches and methods in language teaching* (2nd ed.). Cambridge University Press.

Ringo, L. E. (2025). Effectiveness of Teachers' Classroom Pedagogy in Teaching English in Tanzanian Primary Schools. *Journal of Research Innovation and Implications in*

*Education, 9*(3), 365–375.

Wambua, M. (2022). Teacher competence and communicative approaches in CBC implementation. *Journal of Education and Curriculum Development, 4*(2), 89–106